# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# SHULE YA SEKONDARI KIPINGO S.L.P 29, MALINYI

**Simu No. 0673 345 405 /0717 643 843 /0717 943 092**

Kwa Mzazi / Mlezi wa: ……………………………………………………………………

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIPINGO KIDATO CHA TANO (V) MWAKA 2025 / 2026**

## 1.0 UTANGULIZI.

Ninayo furaha kubwa kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga **Shule ya Sekondari Kipingo** kidato cha tano 2025 katika **Tahasusi ya** ............................ Masomo yataanza tarehe **08/07/2025**, hivyo unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **30/06/2025**. Tarehe ya kufungua / kuripoti shuleni inaweza kubadilika kutegemeana na maagizo ya Waziri mwenye dhamana.

## 2.0 KUFIKA ILIPO SHULE.

Shule ipo umbali wa kilomita 370 kutoka Kituo Kikuu cha Mabasi Msamvu (Morogoro). Panda mabasi yanayotoka Kituo Kikuu cha Mabasi Msamvu kwenda Malinyi mjini. Ukifika stendi Kuu ya Malinyi mjini, panda pikipiki mpaka shuleni. Ukitumia usafiri wa Treni (TAZARA) kutokea Mbeya au Dar es Salaam, shuka Ifakara mji halafu panda gari za Malinyi.

## 3.0 MAMBO MUHIMU YA KUFANYA

Pamoja na kukupongeza kwa kufanikiwa kupata nafasi hii muhimu ya kujiunga kidato cha Tano,ninatumia fursa hii kusisitiza yafuatayo:-

a) **Kusoma kwa** makini maelezo yote yaliyomo kwenye fomu hii ya kujiunga (**joining instructions)** ya Shule hii na kutekeleza bila kisingizio maelekezo yote ili kuleta ufanisi wenye tija katika kukupatia elimu iliyo bora kwa muda wote wa masomo.

b) **Kipingo Sekondari** ni Shule ya bweni kwa wasichana wote wa kidato cha tano na cha sita.

c) **Kujaza** form na: 1, 2 na 3 na kuzirudisha shuleni wakati wa **kuripoti. Fomu na 3 ijazwe na** Daktari wa Hospitali au kituo cha afya cha serikali. Fomu zote zibandikwe picha za *passport size* kama inavyoelekezwa.

## 4.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 4.1 AFYA

a) Kila mwanafunzi anapaswa kuripoti shuleni na kadi ya bima ya afya (**NHIF** au **CHF**), kama hana bima ya afya, mzazi au mlezi hakikisha unamkatia bima ya afya kabla ya kuripoti Shuleni.

b) Kila mwanafunzi lazima apimwe afya yake kabla ya kujiunga na Shule na wakati wowote Shule itakapoona kuna haja na umuhimu wa kufanya hivyo.

c) Endapo mwanafunzi ataugua, ataomba kibali kwa Mwalimu wa Zamu au Mwalimu Mlezi kama ataenda hospitali na kurudi siku hiyo hiyo. **Ruhusa ya kulala nje ya shule itatolewa na Mkuu wa Shule.**

d) Mwanafunzi mwenye tatizo la kiafya kama vile pumu, moyo, kifua kikuu nk. **Lazima** tatizo lake la kiafya lithibitishwe na **daktari wa hospitali ya serikali** ambaye atamshauri mgonjwa na shule kwa **maandishi.**

e) Kila mwanafunzi atatakiwa kula chakula cha shule mesini au maeneo yaliyoruhusiwa na shule.

f) Kila mwanafunzi atapaswa kutunza mwili wake na kuwa safi wakati wote kwa kukata kucha kuoga, kupiga mswaki, kutandika kitanda na kupanga vitu vizuri bwenini. **Hairuhusiwi kuvaa pete ,mikufu, hereni na mapambo mengine ya mwilini.**

### 4.2 SARE YA SHULE

**a)** Sare ya shule iliyo sahihi kwa wasichana ni Shati jeupe mikono mifupi, sketi ndefu **inayofika kwenye kifundo cha mguu cha mwanafunzi** yenye **rangi nyekundu** na marinda ya kupanga yenye upindo (belti) wa inchi mbili, isiyo na mikanda na, **tai nyekundu kama rangi ya sketi ( staili ya kipepeo).** Sketi na tai mzazi ukipenda waweza kuvipata karibu na shule

**b)** Kwa Wanafunzi wanaovaa hijabu, mashati yao ni mikono mirefu na hijabu nyeupe isiyo na urembo wa aina yoyote ya kuvaa sambamba na sare ya shule na sio vilemba au mitandio. Ni muhimu kuhakikisha hijabu inafunika kifua sambamba na viwiko vya mikono. Pia iwe nzito isiyoonesha.

**c)** Viatu vya rangi nyeusi vya kufunga na kamba na visiwe na visigino virefu pamoja na soksi ndefu nyeupe jozi mbili .

**d)** Viatu vijulikanavyo kwa jina maarufu la *simpo* vyenye kuacha sehemu ya miguu wazi **haviruhusiwi** kabisa kuvaliwa shuleni.

**e)** Nguo za michezo ni Tracksuit ya **DARK BLUE** (yenye mistari meupe ubavuni isiyo na maandishi, raba nyeusi na soksi za rangi nyeupe.

**f)** Mzazi unashauriwa kumpatia Mwanao mahitaji ya kutosha kwani hataruhusiwa kutoka nje ya shule kwa muda wote wa masomo.

**g)** Sweta la rangi ya BLUE lenye mtindo wa **V**- shingoni.

### 4.3 MAHITAJI MUHIMU YA BWENI

a) Wanafunzi wa bweni wawe na jozi mbili za sketi ndefu zinazofika kwenye kifundo cha mguu wa mwanafunzi za rangi nyeusi zenye upindo (belti )na zenye marinda ya kupanga zisizo na mikanda.

b) T-shirt ya rangi ya bluu aina ya form six au ukipenda waweza kuipata karibu na shule.

c) Suruali nyeusi mbili (2) **zisizobana** na jaketi la blue lisilo na maandishi au urembo na zitavaliwa usiku wakati wakujisomea (Preparation).

d) Shuka mbili na foronya mbili za rangi za pinki, chandarua (mosquito net) na mto.

e) Taulo moja na nguo za ndani za kutosha

f) Ndoo binafsi mbili za lita kumi .

g) Godoro la futi 2.5 kwa futi sita (2.5x6) na si vinginevyo.
h) Vyombo vya kulia chakula kama vile sahani ,kikombe bakuli na kijiko.
i) Wanaovaa hijabu, watavaa hijabu **NYEUPE** nje ya madarasa sambamba na T-shirt za shule na si vinginevyo.

### 4.4 ANGALIZO

a) Mwanafunzi asije na mizigo au begi kubwa shuleni, aje na nguo zilizoorodheshwa tu na asije na nguo za ziada ambazo hazijaidhinishwa.
b) Mwanafunzi **haruhusiwi kuja na simu shuleni**.
c) Hairuhusiwi mwanafunzi kutembelewa na wageni wakati wote atakaokuwepo hapa shuleni **ISIPOKUWA** kwa wito iwapo atalazimika. Siku ya kuwaona wanafunzi ni siku ya mahafali ya kidato cha nne na cha sita.
d) Ni muhimu kwa mzazi/ mlezi kutoa nafasi kwa walimu kufanya kazi zao bila usumbufu kwa kutomshirikisha mwanafunzi mambo yasiyo na tija kwake akiwa shuleni.

## 5.0 MICHANGO YA SHULE

### 2.3 MICHANGO MBALIMBALI

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Malipo yalipwe kupitia akaunti ya shule, Benki ni **NMB Acc No: 21901100034 JINA: KIPINGO SECONDARY SCHOOL** (***tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye risiti ya malipo na sio jina la mwekaji au mzazi***)

## 6.0 MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI.

**a)** Begi kwa ajili ya kubebea daftari.
**b)** Kila mwanafunzi anapaswa kuripoti na vifaa vifuatavyo vya usafi kulingana na tahasusi yake.

- Mwanafunzi wa HGK ataleta, Jembe moja lenye mpini na hard broom moja
- Mwanafunzi wa HKL ataleta kwanja moja na Mopa moja
- Mwanafunzi wa HGL ataleta reki moja na soft broom moja
- Mwanafunzi wa HGLi ataleta jembe moja la mpini na soft broom moja
- Mwanafunzi wa HGFa ataleta kwanja moja na hard broom moja

**c)** Kila Mwanafunzi atatakiwa kuleta Ream mbili (2) kwa mwaka za karatasi ya photocopy A4 (500sheet 80g/$m^2$ na sio rulled wala duplicating papers).
**d)** Vifaa vya kujifunzia vya kutosha kama vile daftari, kalamu,na vitabu. Kwa wanafunzi wenye somo la Geography waje pia na *scientific caluculator* na *mathematical set.*

e) Ieleweke kuwa **HAIRUHUSIWI KUJA SHULENI NA SIMU,** na mwanafunzi. atakayekamatwa na simu atafukuzwa shule kwa mujibu wa sheria za shule.

f) Ikumbukwe kuwa muda wa kuripoti shuleni mwisho ni saa kumi na mbili na nusu (12:30) jioni.

**NB:** ***Kuepukana na usumbufu unaojitokeza sambamba na kuibiwa, wazazi mnashauriwa kununua vifaa vyote tajwa maeneo karibu na shule kwani huduma za kifedha zinapatikana jirani na shule ilipo.***

## 7.0 SHERIA ZA SHULE.

Shule ya sekondari kipingo inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya Mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na.10 ya Mwaka 1995.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

1. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kiujumla ni jambo la lazima.
2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
3. Kushiriki kwa makini katika kufanya maandalio ya jioni (Preparation).
4. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa / pangiwa.
5. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekeo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako hapa shuleni.
6. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
7. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
8. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
9. Kutunza mali za Umma.

### MAKOSA YAFUATAYO YANASABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE AU KUSIMAMISHWA SHULE.

i. Wizi
ii. Uasherati na Ushoga
iii. Kukataa adhabu kwa makusudi
iv. Kuwa / kumiliki simu ya mkononi
v. Kudharau wimbo wa Taifa na Bendera ya Taifa
vi. Kuoa / kuolewa
vii. Kutoa mimba
viii. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
ix. Kupiga au kupigana
x. Kumpa au kupata ujauzito
xi. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
xii. Ubakaji
xiii. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule na watu.

## 7.1 RATIBA YA SHULE.

Kila mwanafunzi anapaswa kuzingatia kwa makini ratiba ya shule kwa kuwa mahali panapohusika kwa wakati muafaka kipindi chote awapo shuleni.

Kuanzia saa moja kamili asubuhi kila siku za masomo mwanafunzi atakuwa na wajibu wa kufanya na kutekeleza kikamilifu shughuli zifuatazo:

a) Kufanya usafi katika eneo lake alilopangiwa (special area).

b) Awahi mstarini (parade) na kuchukuliwa mahudhurio mapema kengele inapogongwa. Mwanafunzi atakayechelewa au kutokufika msitarini bila kibali maalumu kutoka uongozi wa shule, hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.

c) Kuhudhuria vipindi vyote darasani kwa mujibu wa ratiba ya shule.

d) Ni lazima na sio hiari kwa mwanafunzi kufanya mazoezi yote yanayotolewa walimu ndani na nje ya darasa.

e) Kutii na kuheshimu kengele kwa kuwa mahali panapohusika kwa wakati mwafaka.

## 7.2 MATUMIZI YA SARE ZA SHULE

a) Kila mwanafunzi atatakiwa kuwa katika sare ya Shule kama ilivyoainishwa katika fomu ya kujiunga na shule (joining instruction).

b) Wakati wa michezo wanafunzi wote watakuwa katika sare kamili ya michezo wakati wa ushiriki wao katika michezo husika na si vinginevyo.

c) Wanafunzi wanaruhusiwa kuvaa sweta za rangi ya bluu yenye muundo wa **v** shingoni wakiwa shuleni. **Majaketi hayaruhusiwi.** Wanafunzi wa bweni wavae sare kamili ya shule waanaposafiri kwenda likizo au wanaporudi kutoka likizo.

**Mfano wa rangi ya sketi ya shule**



## 7.3 NIDHAMU

a) Hairuhusiwi kutoka nje ya shule bila ruhusa. Ruhusa ya kutoka nje ya shule inatolewa na Mkuu wa shule kupitia Matroni pamoja na mwalimu wa zamu au Mwalimu darasa husika.

b) Hairuhusiwi kukatiza uzio (trace passing) katika njia isiyoruhusiwa,wanafunzi wote watumie lango kuu kutoka na kuingia shuleni.

c) Hairuhusiwi mwanafunzi kuzurura wakati wa vipindi. Wanafunzi watakaotaka kujisomea (private studies) wanaruhusiwa kuwa maktaba au darasa maalumu litakalotengwa kama ukumbi wa shule utakuwa katika matumizi mengine.

d) Hairuhusiwi kwa wanafunzi kuja na simu ya mkononi shuleni.

e) Mwanafunzi harusiwi kupiga kelele anapokuwa msitarini (parade), darasani au bwenini.

f) Hairuhusiwi mwanafunzi kufuga kucha,nywele na kusuka.

g) Mwanafunzi anapaswa kuwa nadhifu lakini haruhusiwi kutumia vipodozi kama vile wanja,*lipshine*,*eyeshadow*,*cream* n.k.

h) Wanafunzi wawapo shuleni, matibabu yao yatafanyika katika hospitali za umma.

i) Mwanafunzi awapo shuleni hataruhusiwa kutoka nje ya shule isipokuwa siku maalumu(outing day na kwa ruhusa maalumu).

j) Kila mwanafunzi lazima ajue kuimba kwa ufasaha nyimbo zifuatazo:-

- Wimbo wa ‘Taifa’
- Wimbo wa ‘Tanzania nakupenda’
- Wimbo wa ‘shule’
- Wimbo wa ‘Tazama ramani’
- Wimbo wa ‘kuwasha mwenge’
- Wimbo wa ' Jumuiya ya Afrika Mashariki'

## 7.4. SEHEMU AMBAZO WANAFUNZI HAWARUHUSIWI KUFIKA BILA KIBALI.

- Maabara
- Jikoni
- Nyumba za walimu na wafanyakazi.

## 7.5 SEHEMU ZILIZOPIGWA MARUFUKU WANAFUNZI KUTEMBELEA

- Vilabu vya pombe
- Majumba ya starehe(clubs)
- Nyumba za kulala wageni
- Mazingira yoyote yale ambayo mwanafunzi hatakiwi kufika kwasababu za kinidhamu na kiusalama. Mfano kuhudhuria katika sherehe za mitaani / misiba.

## 7.6 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

Makosa yaliyoorodheshwa hapa chini yanasababisha mwanafunzi kufukuzwa shule moja kwa moja.

a) Wizi.

b) Kutohudhuria shule kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.

c) Kugoma na kuhamasisha mgomo.

d) Kuwa na lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,walimu,walezi na jamii kwa ujumla.
e) Kupigana wanafunzi kwa wanafunzi ,kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule.
f) Kusuka nywele,wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shulen.
g) Kufuga ndevu.
h) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.
i) Uvutaji wa sigara.
j) Uasherati,uhusiano wa jinsia moja ,kuolewa.
k) Kupata ujauzito au kutoa mimba.
l) Kushiriki vitendo vya uharifu,siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
m) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
n) Kumiliki,kukutwa au kutumia kadi ya simu au simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
o) Kudharau Bendera na Wimbo wa Taifa.
p) Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
q) Uharibifu wa mali za umma kwa makusudi ikiwemo kuchora/kuandika ukuta ,kuharibu mabomba,viti au meza.
r) Kukataa adhabu kwa dharau au kwa kiburi.
s) Kukutwa nje ya shule bila ruhusa au kibali(utoro).

Kutokana na uhaba wa vitabu mashuleni, mzazi/mlezi kama utapenda kumnunulia vitabu mwanao, vimeorodheshwa hapa chini kulingana na tahasusi ya mwanao:-

1. Vitabu vya Kiswahili,

| **RIWAYA** | **WAANDISHI** |
|---|---|
| • VUTA N’KUVUTE | SHAFI ADAM SHAFI |
| • MFADHILI | HUSSEIN TUWA |
| • KUFIKIRIKA | SHABANI ROBERT |
| • USIKU UTAKAPO KWISHA | MBUNDA MSOKILE |

**TAMTHIRIA**

| | |
|---|---|
| • MORANI | EMMANUEL MBOGO |
| • NGUZO MAMA | PENINA MHANDO |
| • KIVULI KINAISHI | SAID MOHAMMED |
| • KWENYE UKINGO WA THIM | IBRAHIM HUSSEIN |

**MASHAIRI**

| | |
|---|---|
| • CHUNGU TAMU | TEOBAD MVUNGI |
| • FUNGATE YA UHURU | MOHAMED S. KHATIBU |
| • MAPENZI BORA | SHABAN ROBERT |
| • KIMBUNGA | HAJI GORA |

2. Vitabu vya English language

**i. NOVEL**

| | |
|---|---|
| • The beautiful one Are not Yet born | by AYI KWEI ARMAH |
| • The man of the People | Chinua Achebe |
| • Vanishing shadow | Namige kayando |
| • His excellence The head of state | Dan Safo |

**ii PLAYS**

| | |
|---|---|
| • An Enemy of the People | Henrik Ibsen |
| • Betrayal In the City | Fransis Imbuga |
| • I will Mary when I want | Ngugi Wa Thiong'o &Ngugi wa Mirii |
| • Black Mamba | JOHN LUGANDA |

**iii. POETRY**

| | |
|---|---|
| • SELECTED POEM | Tanzania Institute of Education |
| • The wonderful surgeon And other poems | Charles Mloka |

| | |
|---|---|
| 3. History paper 1 & 2 | Salehe Yasini |
| 4. Geography for secondary school form five (V) | TIE |

***KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI KIPINGO***

**FLORA G. MTURANO**
**MKUU WA SHULE**

## FOMU NA. 1: AHADI YA MZAZI / MLEZI

Mimi………………………………………………… S.L.P………. Mji ………………………Namba ya simu…………………..

Ambaye kazi yangu ni ……………………………………. Natamka hapa kama mzazi / mlezi wa ……………………………………………………………Ninakubali kwa hiari yangu mwanangu asome katika shule ya Sekondari KIPINGO kuanzia tarehe ………………………….

Ninaahidi kama ifuatavyo:

1. Kwamba nimekubali alilopewa mwanangu na sitamruhusu kubadilisha hadi apate kibali cha maandishi kutoka kwa mamlaka husika
2. Ninaahidi kumpatia mwanangu vifaa vyote kama vilivyoainishwa katika fomu ya kujiunga ikiwemo SARE KAMILI ya shule bila kuharibu chochote.
3. Ninatambua ya kuwa walimu wanahitaji ushirikiano wangu katika kumpatia mwanangu Elimu na nitashirikiana bega kwa bega kwa maswala yanayomhusu mwanangu kitaaluma na Nidhamu ili aweze kufikia malengo yake na Taifa.
4. Naahidi kuwa endapo mwanangu ataenda kinyume na taratibu zilizoainishwa katika fomu hii achukuiliwe hatua stahili za kinidhamu kama alivyoorodheshewa.

Uhusiano wangu na mwanafunzi : …………………………………………….

Jina : ……………………………………………………………… Sain : …………………… Tarehe : ............................

## AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi mwanafunzi……………………………………………wa kidato cha tano chaguo ................. (tahasusi) mwaka 2025/2026.Ninakiri kusoma,kuelewa na kuahidi kutii taratibu zote zilizoainishwa katika fomu iliyotumwa kwangu na mkuu wa shule ya sekondari KIPINGO. Nitatoa ushirikiano wa kutosha kwa walimu wangu na shule kwa ujumla katika muda wangu wote nitakaokuwa shuleni ili niweze kupata elimu na kuendeleza jamii na Taifa langu.

Jina :…………………………………………………… Saini :.................................Tarehe : ……………..

**FOMU NA 2: KIAPO CHA MZAZI/MLEZI**

Mimi…………………………………………………….……….. wa ……………….....……………… S.L.P………………
Namba ya simu : .......................................................Nakiri kukaa na kuzungumza na mwanangu juu ya taratibu za shule na ninaahidi kumsaidia na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa mkuu wa shule na walimu kwa muda wote ambao mwanangu atakapokuwa katika shule hii.Ninatambua madhara ya mwanangu kutembelewa na wageni wasioeleweka wakati akiwa shuleni na ninaomba shule iwatambue watu wane (4) ambao wanahusika katika muda wote ambao atakuwa shuleni nao ni: (ambatanisha picha passpoti size zao).

1. Jina ……………………………………………….
   Simu …………………….
   Uhusiano……………………….

2. Jina ……………………………………………….
   Simu …………………….
   Uhusiano……………………….

3. Jina ……………………………………………….
   Simu …………………….
   Uhusiano……………………….

4. Jina ……………………………………………….
   Simu …………………….
   Uhusiano……………………….

**Saini ya mzazi/mlezi :………………………………….**

**Simu :……………………………..** **Tarehe :………………….**

**FOMU NA 3: UTHIBITISHO WA AFYA**

PICHA

KIPINGO SECONDARY SCHOOL

P.O.BOX 29

MALINYI.

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

To be completed by medical officer from a known public hospital or Health centre in respect to all entrants

Full name……………………………………………….Age…………………..sex……………..year…………………..

1. Blood count (red and white) ……………………………………………………………….............
2. Urine analysis Test……………………………………………………………………………..........
3. Syphilis test……………………………………………………………………………………….....
4. T.B…………………………………………………………………………………………..............
5. EYE TEST………………………………………………………………………………….............
6. Ears………………………………………………………………………………………………...
7. Spleen……………………………………………………………………………………………...
8. Abdomen…………………………………………………………………………………………..

ADDITIONAL INFORMATION: Eg physical impairment, family disease chronic infection etc.

……………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………

I certify that the above named individual is fit to pursue studies as stated above

………………………………… ……………………………………………………

Name and Designation Signature and official stamp

……………………………………….. ……………………………………………………

STATION DATE

NOTE:

1. Medical officer during the course of this examination please attend the individual according to any diagnosed case.

   The dull filled form must be handed to the head of school during registration week, under no circumstances should a student be registered without certification of his/her physical fitness